

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**



**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA  
SEKONDARI ZA SERIKALI**

**Shule ya Sekondari MBAMBA BAY**

**S.L.P 41 MBAMBA BAY**

**Tarehe 4/05/2026**

**Namba za Simu 0755926429**

**Mkuu wa Shule 0765605693/0782364803**

**Makamu Mkuu wa Shule 0766196180/0716278422**

**Matron/Patron 0621902607/0622326409/0740811321**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .....**

**S.L.P .....**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MBAMBA BAY HALMASHAURI YA NYASA MKOA RUVUMA**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya .....

Shule ya Sekondari MBAMBA BAY ipo umbali wa Kilometa 6 Magharibi mwa Mji wa MBAMBA BAY Usafiri wa pikipiki au bajaji kutoka mjini unapatikana kwa sh. 3000 tu. Aidha Usafiri wa basi kutoka Dar es salaam Kuja Mbinga ni kila siku kwa basi la Selous, Superfeo na SAMAs. Aidha mabasi ya SAMAs, SuperFeo, Selous, New Force na Maning Nice hutoa huduma kila siku kutoka Dar es salaam kuja Songea pia kutoka Mbeya ni kila siku mabasi ya Superfeo. Kutoka Dodoma kuja Songea na Mbinga tumia Superfeo na Shabiby kila siku. Aidha Songea mjini hadi Mbamba bay usafiri unapatikana katika kituo cha mabasi Ruhuwiko Songea mabasi ya Kisumapai, Kangaulaya, Lipaya na

mengine, nauli ni shilingi 14,000/= tu, (kutoka mjini Mbinga hadi Mbamba bay nauli niTsh. 7,000/= mabasi ni mengi.

Muhula wa Masomo utanza tarehe ..... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe .....

## **1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

### **Sare za Shule**

- I. Sketi ya shule rangi ya chocolate ( kahawia) mshono ni rinda boksi mbele na nyuma, ndefu inayofunika viatu ( sketi 2)
- II. Rangi ya hijab (kijuba) – nyeupe kwa wale wenye imani ya dini ya kiislamu, ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (vijuba 2)
- III. Shati jeupe mikono mirefu ( mashati 2)
- IV. Sare ya michezo kwa shule hii ni traksuti ya blue yenye lenda nyeupe isiyobana mwilini, ,t-shirt ya bluu na raba nyeupe
- V. Viatu vya shule ni ngozi nyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
- VI. Soksi jozi mbili nyeupe za shule
- VII. Blazia nyeupe za kutosha
- VIII. Nguo za ndani za kutosha
- IX. Sweta-rangi ya chocolate (kahawia) shingo ya V
- X. Nguo za kushindia (shamba dress) gauni refu mshono wa solo rangi damu ya mzee na kijuba cha rangi ya damu ya mzee (kwa wenye imani ya uislamu)
- XI. Tai ya kufunga ndefu rangi chocolate ;
- XII. T-shirt yenye nembo na moto wa shule hupatikana shuleni kwa sh. 12,000 tu
- XIII. Kandambili/ndala au yebo yebo kwa ajili ya kuogea
- XIV. Kanga doti moja kwa ajili ya kuogea
- XV. Taalo la kujifutia baada ya kuoga
- XVI. Picha passport za ndugu 4 wanaoishi karibu na shule
- XVII. Taalo za kike(pads) bunda 6 au zaidi

## 2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

- i. Madaftari 15 quire 3 au 4
- ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
- iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
- iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
- v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma mathematics, chemistry, economics na Geography;
- vi. Mwanafunzi aje na godoro futi 2 ½ x6x4. Kwa atakayependa yanapatikana jirani na shule kwa gharama ya shilingi 45,000/= banko au Dodoma kwa shilingi 54,000/=
- vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya bluu au nyeupe
- viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe); vya bati
- ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
- x. Kwanja 1, jembe 1, mopa 1, fagio laini 1, panga 1, chelewa 1 brashi ngumu ya kusugulia chooni 1.
- xi. Koti la maabara 1 (lab.coat) rangi nyeupe kwa wanaosoma masomo ya sayansi
- xii. Koti la mvua jeusi (rain coat) au mwamvuli

### 2.1 Michango mbalimbali

Na	Aina ya Mchango	Kiasi
1.	Mchango wa Uendeshaji wa Shule	65,000/=
3.	Tahadhari	5,000/=
4.	Nembo	5,000/=
5.	Kitambulisho cha Shule	5,000/=
	<b>Jumla</b>	<b>80,000/=</b>

**Michango yote ilipwe benki kwenye Akaunti ya shule NMB 61701200123 MBAMBA BAY SECONDARY SCHOOL.**

3. Kila mwanafunzi anatakiwa aje na BIMA ya Afya kwa ajili ya matibabu. Kwa mwanafunzi ambae hana bima ya afya anatakiwa kuja na kiasi cha tsh. 50,400/= tu taslimu siku anapowasili ili apewa kadi ya Bima ya afya kwa mwaka mmoja.

Kabidhi risiti ya benki kwa mhasibu ili upewe risiti ya shule pindi utakapofika shuleni.

## **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebisha kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### **3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- ix. Kutunza mali za shule;

- x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

- i. Wizi;
- ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
- vii. Kufuga ndevu;
- viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

- ix. Uvutaji wa sigara;
- x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
- xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
- xii. Kusababisha mimba;
- xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
- xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

**1. FOMU YA KUKUBALI AU KUKATAA KUJIUNGA NA SHULE HII**

**1.1 MWANAFUNZI**

i. Majina kamili (matatu)

.....  
...

ii. Shule ya O-Level aliyosoma

.....

iii. Namba ya mtihani (CSEE)

.....

....

iv. Tarehe ya kuzaliwa

.....

.....

v. Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa (kata lisilohusika)

vi. Nakiri/naahidi kutomiliki au kutumia simu shuleni, kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai.

Sahihi ya mwanafunzi .....

**1.2 MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

a) Nakubali mwanangu apate elimu yake hapo shuleni

b) Na kwamba afuate sheria na maelekezo yote, vinginevyo aadhibiwe

c) Na kwamba mwanangu alelewe katika dini ya

.....

d) Na kwamba siafiki yeye kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

e) Na kwamba nitampa mahitaji yote yaliyoainishwa

f) Na kwamba sitomhamisha mwanangu bila sababu ya msingi

**1.3 AFISA MTENDAJI WA KATA/KIJIJI/MTAA**

Jina ..... Kijiji/kata/mtaa

.....

Wilaya .....

Mk.....

Nathibitisha kuwa mwanafunzi ..... ni wa kijiji/mtaa huu na  
ni raia wa  
TANZANIA  
Saini na  
Mhuri.....tarehe.....

**2. TAARIFA KAMILI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili

.....  
.....

2. Tarehe ya kuzaliwa ..... Dini .....  
Dhehebu .....

3. Mahali ulipozaliwa

.....

4. Shule ya msingi uliyosoma ..... mwaka  
uliomaliza.....

5. Shule ya sekondari uliyosoma ..... mwaka  
uliomaliza .....

6. Kidato unachokuja kuingia hapa Mbamba bay Sekondari

.....

7. Jina la Baba/mlezi..... Uhusiano

.....

Kazi ya baba/mlezi .....

Dini.....

.Namba ya simu ..... E-mail

.....

Anuani

.....

.....

Kijiji/Mtaa/kitongoji/Na. ya  
nyumba.....

Kata ..... Tarafa ..... wilaya ..... Mkoa

.....

8. Jina la mama/mlezi

..... Uhusiano

.....

Kazi ya baba/mlezi ..... Dini

.....

Namba ya simu ..... E-  
mail.....Anuani

.....

...

Kijiji/Mtaa/kitongoji/Na. yanyumba

.....

Kata ..... Tarafa ..... wilaya .....

Mkoa .....

9. Kazi yoyote ya uongozi uliyowahi kufanya:-

Madaraka/UongoziMahali Mwaka

.....

.....

.....

10. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi; kama-Baba, Mama, Dada, Kaka,  
Mjomba, Shangazi nk.

JINA LA NDUGU UHUSIANO KAZI ANAYOFANYA ELIMU YAKE SIMU NA.

.....

.....

.....

.....

Nathibitisha kwamba, habari zilizotolewa hapo juu ni sahihi, naahidi kuwa na  
tabia njema, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

Tarehe..... Sahihi ya mwanafunzi

.....

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

(To be filled by the government medical officer)

Name of the student .....

Date .....

I shall be very grateful if you kindly examine the above named student and give us a report regarding her fitness to undertake studies well in our school.

**A. PRELIMINARY INFORMATIONS: MEDICAL INFORMATION**

S/N	DISEASE	YES	NO	S/N	DISEASE	YES	NO
1	Tuberculosis			9	Operation		
2	Asthma			10	Eye disorder		
3	Pneumonia			11	Diabetes		
4	Heart trouble			12	Nervous breakdown		
5	Recurrent indigestion			13	Ear/Nose/Throat trouble		
6	Kidney trouble			14	Skin disorder/disease		
7	Anemia			15	V.D		
8	Jaundice			16	Disabled		

**VITAL STATUS**

Age ..... Height ..... Weight ..... Blood group .....

Blood pressure ..... Pulse rate ..... systolic ..... Diastolic .....

**MEDICAL EXAMINATION**

	REMARKS/TREATMENT
EAR	RT                      LT
VISION	RT    EYE              LT
THROAT	
CHEST EXAMINATION	
ABDOMINAL EXAMINATION	LIVER                                      SPLEEN

OTHER COMMENTS	
M.S SYSTEM	UPPER LIMBS
	LOWER LIMBS
	SKIN
ANY OTHER FINDINGS	

LABORATORY EXAMINATION/INVESTIGATION

1. STOOL: OVA.....Leucocytes .....
2. URINALYSIS: Protein .....

Glucose .....

Sediment: OVA .....

Leucocytes .....

Hb.....

Bs.....

VDRL.....

WBC Total .....

Differential

N.....L.....

M.....E.....

B.....

X-ray chest (if any).....

ANY OTHER INVESTIGATION

.....

.....

MEDICAL CERTIFICATION

I have examined the above named student considered that he or she is physically fit/unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.

Date ..... station.....

Doctor's name .....

Signature.....

Thank you in advance

.....  
Z.A. MSAMBWA  
THE HEADMASTER  
0755926429/0769582662

## ORODHA YA VITABU

### HISTORY

Major Issues in Africa ICD

- Major events in African History Mwaijage
- The political economy Imperialism Nabudere
- Aa Sinccce 1800. 4th edition Roland Oliver Atmore
- The making of Modern Africa. Vol.1
- How Europe under developed Africa Walter Rodney
- The 20th century Duff, M.N
- Europe from 1815 Pea Cock

### 2) GEOGRAPHY

- Certificates of Geography (Oxford) by Marry Mugo ,Robert Karuggah ,Paul Kibuuka
- General Geography in Diagrams R.B. Bunnet
- Regional Geography Nyngwine/Msabila
- Photograph interpretation S.E. Dura
- Elementary Surveying for Secondary level, New edition
- Certificate of human and Economic Geography Morgans and Leong Chang
- Principles in Physical Geography Monk House

□ Geography-An Intergrate Approach David Waugh (2009)

□ Practical Geography Pritchard

### 3) ENGLISH LANGUAGE

#### PART ONE

a) A Complete English Course for Form Six Michael Kadegehe

b) English for Form V and VI G. Broughton

c) Teaching English as a Foreign Language L.G

d) Longman Grammar

e) Advanced Learner's Dictionary Oxford University Press

#### PART TWO

#### NOVELS

a) The Beautyful One's are Not Yet Born A.K. Amah

b) The Grain of Wheat NgugiwaThiong'o

c) A Man of the People Chinua Achebe

d) Vanishing Shadow N. Kayombo

e) His Excellency the Head of State

#### PLAYS

a) Betrayal in the City

b) An Enemy of the People

c) LwandaMagere

d) I will Marry when I want

#### POETRY

a) Selected poems

b) Growing up with poetry

c) Summons

### 4) KISWAHILI

□ TAMTHILIYA

a) Morani

b) Kivuli kinaishi

c) Kwenye Ukingo waThim

d) Nguzo Mama

□ RIWAYA

- a) Usiku utakapokwisha
- b) Vuta N'kuvute
- c) Mfadhili
- d) kufikirika

□ MASHAIRI

- a) Fungate ya Uhuru
- b) Mapenzi Bora
- c) ChunguTamu
- d) Kimbunga

**VITABU VINGINE VINAVYOHITAJIKA**

**A. GEOGRAPHY**

1. Dura S.E- Map Reading
2. D.N. Mc Master-Map Reading for East Africa
3. Pritchard J.M- First lessons in Reading
4. Emilian .c. Knight, L.B. and Hand Weker, M.(1989). Earth Science

**B. HISTORY**

1. Chance .M. and Writte, J.(1950)-Modern World History
2. Boahen, A. (1997)-Topics in West African History
3. Adm, G.(1970). World Civilization
4. Kiruti, F. (2000)-The Evolving World
5. Nigel Kelly and Grey Lacey (2001)-Modern World History
6. Assa Okoth- A History of Africa

**C. ENGLISH LANGUAGE**

1. English for form V and VI Oxford
2. Advance English Revised edition Ashel
3. The Wonderful Surgeon and other poem Charles Mloka
4. Advanced level Literature NyambariNyangwine

**VITABU VYA SAYANSI**

**A. CHEMISTRY**

1. Advanced level Physical Chemistry with General Chemistry (Ape Network)

2. Chemistry for A' level and 1st year undergraduate students Inorganic Chemistry Part A& B(By J.S MARO – AND MIKESEWALLA) Mzumbe Book Project.
3. Conceptual Chemistry, Class XI & XII (By S. CHAND)
4. A' Level Chemistry, 4th Edition (E.N RAMSDEN)
5. Organic Chemistry Part A & B (MZUMBE BOOK PROJECT)

## **B. PHYSICS**

1. Advanced Physics by Tom Duncan 4th edition
2. Advanced Physics by Nelkon and Parker
3. College Physics
4. Principles of Physics for class XI & XII by S. CHAND
5. Advanced Physics (Mechanics 1) by Reznicle.

## **C. MATHEMATICS**

1. Pure Mathematic I & II J.K. BOOK HOUSE
2. Pure Mathematic by C. J TRUNTER
3. Advanced Mathematics S. CHANDLER & L. BOSTOCK
4. Understanding Mathematics by A.J. SADLER
5. Core Mathematics for Advance Level by L. Bo stock & S. Chandler
6. S. Chand's Mathematics for class XI & XII H.K Dass.

## **D. BIOLOGY**

1. Understanding Biology 4st Ed, Glenn and Susan Toole. Stanley Thomes 1999.
2. Biological Science 3rd Ed. D Tylor. NPO Green and Stout
3. Guidance to dissection H.G.Q ROWETT H.
4. Advanced Level Biology, text book form V and VI BY Ernest Kira 2009

## **E. ECONOMICS**

1. Modern Economic by mudida
2. Managerial Economic by oxford
3. Micro Economics by Meconnel Brue.
4. Macro Economics

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## **KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule .....**

**Jina la Mkuu wa Shule .....**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule .....**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO AMBAZO ATAZITUMIA KUWASILIANA Nawe MZAZI: -**

- **Mkuu wa shule 0755926429/0765605693/0782364803**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0716278422/0766196180**
- **Mwandamizi Taaluma 0756635959**
- **Mwandamizi Malezi 0765302618**
- **Mwalimu wa bweni 0621902607**
- **Mwalimu mhasibu 0768808634**